



Kanton Bern
Canton de Berne



Masomo ya kilazima katika mkoa unaongea kijerumani wa Canton Bern Ujumbe kwa wazazi

Elterninformation zur Volksschule Suaheli

Bildungs- und Kulturdirektion



2 Masomo ya kilazima katika mkoa unaongea kijerumani wa Kanton Bern

Ujumbe Kwa wazazi

Yaliyomo

Utangulizi.....	3
Masomo ya kilazima	4
Mfumo wa masomo ya kilazima	5
Kukuzwa na usaidizi	10
Eltern und Volksschule	12
Majukumu na maelezo ya maneno yaliyotumika.....	15

Impressum

Herausgeberin und Copyright:
Bildungs- und Kulturdirektion
Amt für Kindergarten, Volksschule und Beratung
akvb.bkd@be.ch

Auflage 2022
Download: www.be.ch/volksschule

Utangulizi

Brosha hii inatoa ujumbe kuhusu mfumo wa shule za umma wa mkoa wa Canton ya Bern. Zaidi Wanatoa majibu ya maswali yafwatayo:

- Ni vipi Shule za chekechea, shule za msingi na shule za upili wa chini zilivyoundwa?
- Shule inatumaini nini kutoka Kwa wazazi?
- Wazazi wanaweza wakasaidia kiviipi watoto wao wahisi raha shuleni na pia waweze kupata elimu bora?

Walimu na mwalimu mkuu wa shule ya munispaa (Gemeinde)yako watafurahia kutoa ujumbezaidi.

4 Masomo ya kilazima katika mkoa unaongea kijerumani wa Kanton Bern

Ujumbe Kwa wazazi

Masomo ya kilazima

Masomo ya kilazima

Allgemeines

Kama sharti masomo ya kilazima hudumu kwa miaka kumi na moja.

Mda wa masomo ya kilazima huanza (kuingia shule ya chekechea) katika mwaka ule ambao mtoto anatimiza miaka minne mwezi wa Julai tarehe 31. Kwa hiari yao wazazi wanaweza hairisha muda huo hadi mwaka mmoja uf-watao.

Shule hutoa vyombo ya kufundisha na vya kusoma shuleni kwa wanafunzi bila malipo.

Watoto wake na waume hupewa kanuni moja na malengo ya masomo hutumika baina ya jinsia zote.

Masomo ya kilazima ni sawa kwa wanafunzi wote wakizingatia imani za kidini.

Tume ya shule (*Schulkommission*) na walimu wakuu wa kila munispaa wanajukumu la shughuli za shule za chekechea na shule za msingi.

Wazazi wanapochagua kupeleka watoto wao shule za kibinafsi, watag-haramia karo ya shule wenyewe.

Watoto walemavu wenye mahitaji ambayo hayapo katika shule za umma wanaweza hudhuria shule za elimu maalum(*sondeschule*).

Lengo la shule ya kilazima

Ziele der Volksschule

Masomo ya kilazima hutoa msingi mwafaka wa elimu ya jumla na maendelezo ya ujuzi, ambayo itaweka msingi wa masomo ya ujuzi ya siku zijazo, ili kuendeleza msomo katika kitengo cha shule ya upili ya juu Ina masomo ya kimaisha.

Vile vile shule huwezesha kuendeleza ujuzi, hutoa mandhari ya kuheshimiana na kuvumiliana na pia husisitiza wanafunzi kuwa na uwajibikaji kwa wadamu wenzao na mazingira.

Lehrplan 21

Hutumika na walimu kutoka shule ya chekechea hadi mwaka wa 9 kama ramani ya kuwasaidia kupanga mafundisho yao.

Mfumo wa masomo ya kilazima

	Kitengo cha upili cha juu Sekundarstufe II Masomo ya ujuzi na mafunzo au shule ya upili ya juu (Mfano. uanagenzi au uanafunzi au shule ya Baccalaureate)	Miaka 2- 4	
Obligatorische Volksschule	Shule ya upili ya chini (miaka 7-9) Sekundarstufe I Mahitaji ya kitengo cha shule ya upili ya juu Au Mahitaji ya kitengo cha shule ya upili ya chini	Miaka 3	
	Kitengo cha msingi (Mwaka 1-6) Primarstufe	Miaka 6	Kitengo cha msingi Miaka 4
			Basisstufe/ Cycle élémentaire Miaka 3-5
Chekechea Kindergarten	Miaka 2		

Chekecha

Kindergarten

Watoto katika mwaka wa kwanza na wa pili wa chekechea hufunzwa pamoja katika darasa moja. Chekechea huwapatia watoto nafasi ya kuishi kucheza na kukusanya matukio. Lengo lake ni kuchochea na kukuza maendeleo na masomo, vile vile iki-zingatia, mahitaji ya kibinafsi na uwezo na kasi ya kusoma.

Kama amri, watoto wote huingia katika mwaka wa kwanza wa kitengo cha msingi, baada ya kukaa miaka miwili katika chekechea. Katika hali maalum

kutokana na weledi wa mtoto anaweza anza mwaka wa mwanzo wa shule ya msingi, mwaka mmoja mapema au mwaka mmoja kwa kuchelewa.

Katika munispaa zingine watoto wa chekechea hufundishwa pamoja na watoto walio katika miaka yao miwili ya kwanza katika shule ya msingi. (Mchanganyiko wa umri) kwa siku nzima au sehemu ya siku kwa Basisstufe au kwa Cycle élémentaire (tazama jedwali la juu).

6 Masomo ya kilazima katika mkoa unaongea kijerumani wa Kanton Bern

Ujumbe Kwa wazazi

Kitengo cha msingi (miaka 1-6)

Primarstufe (1.–6. Schuljahr)

Kutoka mwaka wa 1 hadi wa 6, wanafunzi hupokea masharti kwa masomo tofauti tofauti kama vile, Lugha (Sprachen), Hisabati (Mathematik) na ujenzi (Gestalten). Wanafunzi huongeza viwango vya kujitegemea na majukumu ya kazi yao na mafunzo.

Kuanzia Mwaka wa 3 wanafunzi katika eneo la kuongea Kijerumani la canton hujifundisha Kifaransa kama lugha yao ya kwanza ya kigeni, katika mwaka wa 5 wanaanza Kingereza vile vile.

Baada ya shule ya msingi, wanafunzi huendelea hadi shule ya upili ya kiwango cha chini. Katika mwaka wa 5, shule huwapatia wanafunzi na walimu habari mwafaka na mikakati ya kuingia shule ya upili ya kiwango cha chini.

Shule ya upili ya kiwango cha chini (miaka 7-9)

Sekundarstufe I (7.–9. Schuljahr)

Katika kiwango cha chini cha shule la upili, wanafunzi hupokea masharti aidha katika kitengo cha mahitaji ya Realschule au kitengao cha mahitaji ya Sekundarschule.

Mahitaji katika kiwango cha Sekundarshule huwa magumu zaidi ya yale ya Realshule.

Wanafunzi hupelekwa katika kiwango wanachofaa na walimu wao kutokana na kuelewa kwao.

Katika muda huu wote wa masharti katika kiwango cha chini cha shule ya upili, kuna msisitizo wa masomo ya ujumla na pia katika uamuzi wa masomo ya siku za usoni na malengo ya kazi. Shule huwa na jukumu la kusaidia katika mikakati ya uamuzi huu, na wanafunzi husaidiwa na kupewa wasia na wazazi wao, walimu na viongozi wa mashauri wanapofanya uamuzi kuhusu njia watakayochukua ya kikazi.

www.be.ch/biz

Baada ya masomo ya kilazima

Nach der Volksschule

Baada ya muda wa masomo ya kilazima wanafunzi hutimiza miaka miwili au minne katika programu ya mafundisho ya kikazi (VET) au kuhudhuria shule ya upili ya kitengo cha juu.

Ujumbe Zaidi kuhusu mwanzo wa VET: www.be.ch/berufsbildung

Tazama tovuti ya chini kwa ujumbe kuhusu Shule maalum ya upili ya juu na Shule ya Baccalaureate
www.be.ch/mittelschulen

Miaka ya shule na muda wa likizo

Schuljahr und Schulferien

Mwaka wa shule huanza kati kati ya mwezi Agosti na kuisha katika mwezi wa Julai. Wanafunzi huunduria wiki 38 au 39 za mafunzo kila mwaka. Katika mwaka wa shule wenye wiki 39, Likizo huazimepangwa ifwatavyo:

- Likizo ya msimu wa Vuli ni mwezi wa Septemba/Octoba: Wiki tatu
- Likizo ya msimu wa baridi ni desemba/januari: wiki mbili
- Likizo ya michezo ni februari: wiki moja.
- Likizo ya masika ni Aprili: wiki mbili.
- Likizo ya majira ya joto ni Julai na Agosti: wiki tano.

Tarehe kamili za likizo ya shule na likizo za Umma (bank holidays), huchapishwa katika tovuti ya shule au ya munispaa.

Ratiba

Stundenplan

Mafunzo haunza Jumatatu hadi Ijumaa. Muda wa somo moja ni dakika 45. Wanafunzi huundhuria angalau masomo matatu asabuhi. Masomo ya asubuhi huanza na kwisha katika muda sawa kwa shule zote za kilazima (wakati wa “block”). Wakati wa alasiri masomo hutofautiana baina ya masomo mawili au manne. Kulingana na mwaka (Kitengo) cha shule na darasa, panaweza kuwa na alasiri moja au zaidi katika wiki ambapo wanafunzi hawana shule somo lolote.

Wazazi wanajukumu la kuhakikisha wanao wanahudhuria shule ipasavyo kulingana na ratiba ya shule.

Wakati wa masomo, shule inalo jukumu la kuhakikisha usimamizi wa watoto.

Nje ya wakati wa masomo na ambapo wanafunzi wanapoelekea au kutoka shuleni, hao huchukuliwa kuwa chini ya jukumu la wazazi wao. Isipokuwa: wakati ambapo shule inawapatia wanafunzi usafiri kwa sababu safari ya kuenda na kurejea shule inatambuliwa kama jukumu nzito kwao mtoto.

8 Masomo ya kilazima katika mkoa unaongea kijerumani wa Kanton Bern

Ujumbe Kwa wazazi

Kutohudhuria na ruhusa iliyo-pangwa ya kutohudhuria

Absenzen und Dispensationen

Mwanafunzi hafai kukosa kuhudhuria shule isipokuwa pale ambapo kutohudhuriwa kwake kumeruhusiwa. Wazazi wanapaswa kupeana habari kwa walimu kuhusu wanao kukosa kuhudhuria shule mbeleni kabisa, Mwishowe kabisa iwe kabla ya somo kuanza. Sababu zinazokubalika za kukosa kuhudhuria shule ni zifwatazo; Kugonjeka kwa mtoto, msiba wa kifo katika familia, kuhama kwa makaazi, au kuenda kwa dakrati au daktari wa meno.

Wazazi wanaweza waondoa-wanao shuleni Kwa muda usiopita siku tano nusu za kadri ya mwaka mzima wa shule bila kuipa shule sababu ya kutohudhuria. Aidha, Mwalimu ni lazima apewe onyo mbeleni.

Mwalimu mkuu wa shule anaweza-peana ruhusa ya kutohudhuria shule inayohusiana na kuadhimisha siku kuu ya kidini, tukio muhimu la kifamilia, kuhudhuria masomo ya lugha ya kuzalia na utamaduni(HSK), au jaribio la mwanagenzi. Ruhusa ya kutohudhuria kuliopopagwa lazima ichukuliwe mbeleni.

Kazi ya ziada

Hausaufgaben

Masomo ya shuleni huendelea wakati wa shule. Kazi ya ziada hutumika kama njia ya kujiandaa kwa au kuka-gua somo. Watoto wanapaswa kufanya kazi yao ya ziada bila usaidizi wa wazazi au mtu yeyote mzima.

Muda wa zaidi wa kazi ya ziada kila wiki:

- Dakika 30, mwaka wa 1 na 2
- Dakika 45 mwaka wa 3 hadi wa 6.
- Dakika 90 mwaka wa 7 hadi wa 9.

Walimu hutayaraisha kazi ya ziada kwa mwanafunzi kulingana na uwezo wa kusoma na weledi wake binafsi.

Tathmini

Beurteilung

Sababu msingi ya Tathmini ni kuchochea kusoma na kukua; nia ni ya kumfanya mtoto kuhisi tathmini ni ya kusoma kwake.

Kila mwaka wa shule mwalimu wa darasa huwaalika wazazi katika mkutano wao wa kibinafsi (*Standortgespräch*). Katika mkutano huu walimu na wazazi hujadili utendaji wa wanao wanavyosoma na weledi wao. Mikutano zaidi inaweza itishwa kwa ombi la wazazi au shule.

Wanafunzi hupokea ripoti za maandishi kuhusu mitihani yao katika mwisho wa 2 wa pili na mwisho wa mwaka wa 4 hadi wa 9. Ripoti hiyo inaangazi weledi wa mtoto katika masomo tofauti. Kuanzi mwaka wa 4, mitihani hupewa Alama za herufi katika ripoti.

10 Masomo ya kilazima katika mkoa unaongea kijerumani wa Kanton Bern

Ujumbe Kwa wazazi

Kukuzwa na usaidizi

Hatua z kuunga mkono

Unterstützende Massnahmen

Watoto walio na asili ya lugha ya kigeni wanaweza kupokea maagizo zaidi katika lugha ya Kijerumani kama lugha ya pili.

Ikiwa mtoto ana uwezo wa pekee wa kikili, anaweza kuhudhuria programu za elimu ya watu walio na vipawa baada ya kupewa tathmini.

Magumu katika kujifunza

Lernschwierigkeiten

Magumu ya kujifunza ya mtoto yanafafanuliwa kukiwa na makubaliano kutoka kwa wazazi na mtaalamu au wakala maalum (ushauri wa kanuni wa elimu). www.be.ch/erziehungsberatung

Elimu rahisi ya mahitaji maalum

Einfache sonderpädagogische Massnahmen

Hatua rahisi za elimu kama vile usaidizi shirikishi, mazoezi ya usemi, hutumika kusaidia wanafunzi kisaikologia kuhudhuria shule ya kawaida.

Watoto walio katika mwaka wa 1 ambao wanahitaji muda zaidi wa kujifunza mambo wanaweza kujifunza mambo hayo katika muda wa miaka miwili.

Ikiwa watoto hawatafikia malengo ya kujifunza licha ya kupewa usaidizi, wanaweza kufundishwa na kutathminiwa kulingana na malengo ya kujifunza ya mtu binafsi.

Darasa maalum

Besondere Klassen

Katika munispaa mingi, watoto walio na upungufu wa kuelewa masomo walio katika kitengo cha msingi au cha upili cha chini, wanaweza hudhuria darasa za masomo maalum

(*Besondere Klasse*). Idadi ya wanafunzi katika darasa maalum huwa kiwango kidogo ili kuwezesha mwalimu kuwapa watoto umakini zaidi wanaposoma.

Elimu inayotekelezwa ya mahitaji maalum

Verstärkete sonderpädagogische Massnahmen

Kwa watoto ambao hawawezi kusomesha vya kutosha na aina hii ya usaidizi, kuna hatua maalum za elimu zilizoimarishwa - katika shule ya msingi ya kawaida au katika shule maalum ya msingi.

Shule ya kutwa

Tageschule

Munispaa huweka shule za kutwa Kwa wanafunzi wanaohitaji usimamizi nje ya masaa ya shule:

- Usimamizi kabla ya masaa ya kuanza shule ya kila siku.
- Usimamizi wakati wa mchana, na chakula cha mchana hupeanwa.
- Usimamizi wakati wa alasiri ambapo masomo ya siku yanapoisha au alasiri ambapo hawapo shuleni.

Masomo ya kutwa sio ya lazima. Wazazi ambao wangependa kuwapelika wanao shule za kutwa itawabidi kulipa ada kulingana na mapato yao, mali na ukubwa wa familia.

Kwa ujumbe wa ujumla kuhusu shule ya kutwa angalia:
www.be.ch/schulergaenzende-angebote

Wazazi wanaweza pokea ujumbe kuhusu fursa za shule zingine za kutwa (Vituo vya hifadhi vya watoto, wataalam wa utunzaji n.k) kutoka kwa munispaa:
www.fambe.sites.be.ch

Kazi ya kijamii shuleni

Schulsozialarbeit

Mfanyakazi wa kijamii wa shule huwapatia usaidizi na wasia kwa watoto wanaobalehe, wanaopitia shida za kijamii au shida za kibinafsi. Walimu, walimu wakuu na pia wazazi wanaweza tafuta ushauri katika ofisi ya kijamii.

Afya

Gesundheit

Wanafunzi wote lazima wapitie ukaguzi wa afya katika mwaka 4 na wa 8. Ukaguzi huu ni wa lazima wa bila malipo.

Wanafunzi wote lazima wapitie ukaguzi wa meno kila mwan uluifanywa na daktarin wa meno wa shule. Ukaguzi huu ni wa lazima wa bila malipo.

Wazazi watapewa ujumbe iwapo daktari au daktarin wa meno atahisi kuwa kuna hitaji la kubaini au matibabu.

12 Masomo ya kilazima katika mkoa unaongea kijerumani wa Kanton Bern

Ujumbe Kwa wazazi

Eltern und Volksschule

Kushirikiana

Zusammenarbeit

Wazazi na walimu wanapaswa, kulingana na sheria kushirikiana. Kubalishana ujumbe wa mara kwa mara na mapatano ya ujumla, uaminifu na heshima ni vitu vya maana katika ushirikiano huu.

Kupeana ujumbe

Gegenseitige Information

Shule kwa kawaida itawapa wazazi ujumbe kuhusu matukio ya maana na mipangilio kuhusu masomo (*matukio, safiri za shule n.k*) au mwongozo wa shule. (*zoezi, kwa shule ama darasa, wakati wa masomo, vyombo vya kufundisha, kanuni za shule n.k.*) Ujumbe huu hutolewa kwa maandishi au katika mikutano ya jioni ya wazazi (*Elternabenden*).

Mikutano ya kibinafsi baina ya walimu na wazazi (*Standortgespräche*) ni muhimu kwa Kushirikiana baina ya shule na wazazi.

Wazazi wanayo haki ya kuhudhuria somo lolote baada ya mipangilio ya awali na mwalimu.

Wazazi wanaombwa kuwaarifu walimu iwapo mtoto anaugua ugonjwa wowote, iwapo mtoto anahitajika ku-meza dawa mara kwa mara au wakati ambapo kitu au jambo ambalo lina-weza kuzuia maendeleo ya mtoto au uwezo wake kuwa makini.

Utafsiri

Übersetzung

Ni muhimu wazazi kuelewa kinachozungumziwa katika mikutano ya jioni ya wazazi na katika mikutano ya wazazi na walimu. Pia ni muhimu wazazi kuweza kujieleza maswala yao na pia kuuliza maswali. Iwapo weledi wa kijerumani au kifaransa wa wazazi si wa kutosha, wanaweza kuomba mkalimani.

Maamuzi ya maana

Wichtige Entscheide

Maamuzi yote yanayohusiana na njia ya elimu ya mtoto (*kusonga kutoka shule ya msingi hadi ya upili ya chini, kwa mfano kupelekwa kwa darasa maalum*) yanajadiliwa na mtoto na wazazi.

Wazazi wanayo haki ya kupewa ujumbe, kupewa wasia na walimu wa wanao na mwalimu mkuu. Wazazi wana haki ya kukagua faili zote zinazo wahuu wanao. Mwalimu mkuu ndiye anayefanya uamuzi kuhusu njia ya elimu ya mwanafunzi na kufanya mawasiliano kwa wazazi kupitia maandishi, yakiwa na mafafanuzi ya uamuzi huo. Iwapo mzazi hawakubaliani na uamuzi huo, wanayo haki ya kuwasilisha malalamishi kwa inspectoreti wa shule (*Schulinspektorate*) kabla ya siku 30 za kuarifu kutimia.

Kuhusika kwa wazazi

Mitwirkung der Eltern

Shule nyingi zina kamati ya wazazi inayowajumuisha mzazi mmoja au wawili kutoka kila darasa. Kamati hii ni ya wazazi wenyewe na huwa inachaguliwa na wazazi kutoka katika kila darasa mwanzoni mwa mwaka wa shule. Wawakilishi wa wazazi hufanya kazi kwa karibu na mwalimu wa darasa. Kamati ya wazazi huhakikisha mawasiliano baina ya wazazi na walimu.

Wazazi wanaweza wakatapa ujumbe zaidi kuhusu kuhusika kwa wazazi katika shule ya chekechea au katika shule kutoka kwa mwalimu wa darasa au mwalimu mkuu wa shule.

Shida shuleni

Probleme in der Volksschule

Pengine mtoto hana utulivu darasani ama weledi wake darasani umezorota kwa ghafla. Mtoto anaweza kuwa anapitia shida na watoto wengine, au wazazi wake hawakubaliani na uamuzi wa mwalimu.

Hatua ambazo wazazi wanaweza chukua:

So gehen Eltern vor

1. Wazazi na walimu wanafaa kuimarisha mawasiliano baina yao. Wajadiliane Pamoja na watafuta njia ya kufikia uamuzi. Mara nyingi, njia hii hupelekea uamuzi wa kuridhisha.
2. Iwapo wazazi na mwalimu hawatapata suluhisho mwafaka, na mmoja wao au wote wanaona inafaa, mkutano utafanywa baina ya wazazi, mwalimu mkuu na mwalimu anayehusika.
3. Wakati wowote, inawezekana kupata usaidizi maalum wahusikao, kama vile ofisi ya maswala ya kijamii ya shule au ofisi ya cantoni ya wasia ya elimu.
4. Iwapo uamuzi hautaafikiwa bado, wazazi wanaweza wasilisha malalamishi katika inspektoreti ya shule.

Shule inaweza alika mtafsiri iwapo atahitajika.

14 Masomo ya kilazima katika mkoa unaongea kijerumani wa Kanton Bern

Ujumbe Kwa wazazi

Kuhamia cantoni ya Bern

Zuzug in den Kanton Bern

Watoto walio na miaka 4 na wenye miaka 15/16 wanahitajika na sharia kuhudhuria shule bora wawe nchini Uswizi na wana nia ya kubaki kwa muda wa miezi kadhaa.

Wazazi ambao wamehamia cantoni ya Bern hivi karibuni wanaweza pata ujumbe kuhusiana na elimu kutoka kwenye munispaa (*Gemeinde*) au kutoka kwenye tovuti ya shule ya eneo la makao yao.

Wanafunzi wenye shida ya lugha wanaweza pata usaidizi zaidi wa kujifundisha lugha.

Wanafunzi wenye miaka 13 ama zaidi ambao hawana ufahamu wowote kuhusu lugha ya masomo wanaweza hudhuria masomo ya lugha kwa mapana ya eneo (*Regionaler Intensivkurs PLUS, RIK+*).

Ujumbe zaidi unaweza patikana kwa www.bkd.be.ch/migration

Majukumu na maelezo ya maneno yaliyotumika

Idara ya elimu

Bildungs- und Kulturdirektion

Ni idara ya elimu katika catoni na uongozi wa elimu. Inaelezea mfumo wa elimu ya kilazima katika munispaa na inatoa mtaala.

Insepektoreti ya shule

Schulinspektorat

Ni mwongozo wa cantoni unaosimamia elimu ya kilazima.

Munispaa

Gemeinde

Munispaa inalojukumu la kupanga elimu ya kilazima katika jamii. Inatoa miundo mbinu ya elimu: majumba ya shule, fanicha na vyombo vya kufundisha.

Tume ya shule

Schulkommission

Tume hii inahakikisha kwamba watoto wanahudhuria shule ya chekechea na shule ujumla kwa kuzingatia masharti ya cantoni na maazimio ya munispaa. Pia inalo jukumu la maamuzi ya mikakati ya shule.

Kiongozi wa shule

Schulleitung

Kiongozi wa shule ana jukumu la kundesha shule. Mbali na majukumu mengine, yeye ndiye anawapa darasa wanafunzi na ana jukumu la uamuzi kuhusu njia ya kielemu ya mwanafunzi.

Mwalimu wa darasa

Klassenlehrperson

Mwalimu wa darasa ndiye mwenye jukumu la elimu na mpangilio kuhusu uongozi wa darasa. Yeye ndiye mtu wa kwanza anayejua ujumbe kuhusu maswala yanayohusika na mtoto wako kuhudhuria chekechea na shule.

